

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA - MIKINDANI



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. MM/MC/S.2/13/168

Tarehe: 22/07/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani anawatangazia waombaji wote wenye sifa kuleta maombi ya kazi kwa nafasi ya Mtendaji wa Mtaa III baada ya kupata idhini ya kutekeleza Ikama na Bajeti kwa Ajira mpya katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa barua yenye Kumb. Na.FA.170/362/01“A”/40 ya tarehe 27 Juni , 2022 , kutoka kwa Katibu Mkuu UTUMISHI, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hivyo basi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa wataanzania wote wenye sifa kuomba nafasi ifuatayo:-

MTENDAJI WA MTAJA DARAJA LA III (NAFASI 5)

1. Sifa za kitaaluma za mwombaji.

- a) Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI)
- b) Aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti (NTA Level 5) katika moja ya fani zifuatazo:- Utawala, Sheria, Rasilimali watu, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo- Dodoma au Vyuo vingine vinavyotambuliwa na Serikali.

2. Mshahara.

Ngazi ya mshahara TGS B1

3. Majukumu ya Mtendaji wa Mtaa Daraja III

- i. Katibu wa kamati ya Mtaa.
- ii. Mtendaji Mkuu wa Mtaa.
- iii. Mratibu wa utekelezaji wa sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa.
- iv. Mshauri wa kamati ya Mtaa kuhusu Mipango ya maendeleo katika Kata.
- v. Msimamizi wa Utekelezaji wa Sheria ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa.
- vi. Mshauri wa kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama.
- vii. Msimamizi wa Utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na Umaskini katika Mtaa.
- viii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
- ix. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Mtaa:

4. MASHARTI YA JUMLA

- i) Waombaji wawe ni raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 na usizidi 45.
- ii) Waombaji wawasilishe picha mbili za hivi karibuni.
- iii) Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Curriculum Vitae) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- iv) Waombaji waambatanishe nakala ya vyeti vya masomo na taaluma, Cheti cha kuzaliwa. Muombaji atakayewasilisha "Result slip" "statement of results" "Provisional results" au "Transcript". Maombi yake hayatapokelewa
- v) Kwa waliosoma nje ya nchi elimu ya kidato cha nne na kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitahani la Tanzania (NECTA).
- vi) Kwa waliomaliza vyuo nje ya nchi wawasilishe uthibitisho kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).
- vii) Waombaji waandike namba ya NIDA katika barua ya maombi au waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Uraia (National Identification Number) kutoka Mamlaka ya vitambulisho (NIDA)
- viii) Waombaji watakaokidhi sifa zinazotakiwa ndio pekee watakaoitwa katika usaili..
- ix) **Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 05/08/2022 saa 9:30 Alasiri.**

MUHIMU: Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu na nyaraka zote zinazohitajika. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa,
S.L.P 92,
MTWARA-MIKINDANI

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri
www.mtwaramikindanimc.go.tz .

Tangazo hili limetolewa na:-



COL Emanuel H. Mwaigobeko
MKURUGENZI WA MANISPAA
MTWARA-MIKINDANI

